

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA TATU**

**KIKAO CHA TISA**

**14 APRILI, 2021**



# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA TISA – TAREHE 14 APRILI, 2021

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

69. **MHESHIMIWA SHAABAN OMAR**  
● **SHEKILINDI (LUSHOTO):** ●

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Jimbo la Lushoto lina Kituo kimoja cha Afya; na sasa Wananchi wameanza kujenga Vituo vya Afya viwili vya Gare na Ngwelo: -

Je, Serikali ipo tayari kutoa fedha kwa ajili ya kumalizia Vituo hivyo na ni lini itafanya hivyo.

70. **MHESHIMIWA MRISHO MASHAKA GAMBO (ARUSHA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga stendi ya kisasa Jijini Arusha ili kukidhi mahitaji ya Wananchi.

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

**71. MHESHIMIWA ESTHER NICHOLAS MATIKO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, ni lini Mnada wa Mifugo wa Magena uliopo Halmashauri ya Mji wa Tarime utafunguliwa kama ambavyo Serikali iliahidi Mwaka 2016.

**WIZARA YA MAJI:**

**72. MHESHIMIWA NICODEMAS HENRY MAGANGA (MBOGWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka Wilayani Mbogwe maji kutoka Ziwa Victoria kwa ajili ya matumizi ya Wananchi.

**73. MHESHIMIWA ALLY MOHAMED KASSINGE (KILWA KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itaanza kutekeleza mradi wa maji kutoka Mto Mavuji kwa ajili ya Wakazi wa Miji Midogo ya Kilwa Kivinje na Kilwa Masoko.

## **WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

### **74. MHESHIMIWA JUDITH SALVIO KAPINGA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutenganisha fedha za maendeleo ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Fedha za Bodi ya Mikopo kwa kuzitengea Vote tofauti fedha hizi za mikopo ili kuleta tija ya miradi ya maendeleo.

## **WIZARA YA KILIMO:**

### **75. MHESHIMIWA DKT. OSCAR ISHENGOMA KIKOYO (MULEBA KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

(a) Je, ni lini miradi ya kilimo cha umwagiliaji ya Kyamyorwa na Buhangaza iliyopo Wilaya ya Muleba itakamilika na kuanza kutumika;

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuendeleza Bonde la Mto Ngono kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji.

## **WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

### **76. MHESHIMIWA NICHOLAUS GEORGE NGASSA (IGUNGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, ni lini Serikali itatoa eneo la Hifadhi ya Bonde la Wembere kwa Wananchi wa Igunga kwa ajili ya kufanya shughuli za kilimo na ufugaji ili kumaliza mgogoro wa muda mrefu katika eneo hilo kwa kuwa Bonde hilo limepoteza sifa ya kuwa Hifadhi.

## **WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:**

### **77. MHESHIMIWA WANU HAFIDH AMEIR (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha elimu ya Sheria zinazowapa kinga na haki Wanawake inatolewa kwa Wanawake wote Mijini na Vijijini.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**78. MHESHIMIWA MWANTUM DAU HAJI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Polisi wa Wilaya Kusini Unguja.

**III. HOJA ZA SERIKALI:**

**WAZIRI MKUU:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

*(Majadiliano yanaendelea)*

**DODOMA  
14 APRILI, 2021**

**S. KAGAIGAI  
KATIBU WA BUNGE**